

Kama wewe ni **kipofu** au **una matatizo ya kuona vizuri** na kama unataka kujua njia tofauti za kuweza kuona, basi tuanze!

Ujuzi na uwezo wa kutambua vitu ni muhimu katika **kuleta mabadiliko katika maisha yako**, kujua malengo yako, na kuwa tayari kufanya kila uwezalo katika kutimiza malengo hayo. Kuwa na vifaa vinavyohitajika, kujua jinsi ya kuvitumia na kuwa tayari kuchukua hatua zinazotakiwa kutakusaidia kufikia kule ambacho unaweza kukifanya.

## **Yote ni katika kuwa huru:**

Jifunze jinsi ya kujishughulikia mwenyewe na kufanya shughuli zote bila ya vipingamizi - nyumbani, shuleni kazini na hata katika michezo.

## **Hii inakuwaje?**

Kila mtu anakuwa na mazingira tofauti. Hivyo mtu mwenye matatizo hukutana na mtaalamu kuweza kutambua malengo yake na kwa pamoja mnaandaa mpango wa utekelezaji.

## **Huduma zinatofautiana kulingana na mahitaji:**

Iwe ni kupata elimu, kusoma kwa kazi maalum, kupata kazi au kuendelea na kazi yako au pia kuweza kuendelea kufanya mambo yako nyumbani bila ya vipingamizi, nguvu zako zikiambatanishwa na huduma zinazotolewa zitakusaidia kupata mafanikio katika kupunguza vipingamizi vinavyotokana na ukosefu wako wa kuona.

## **Tunatoa:**

Ushauri na maelekezo

Tathmini ya ujuzi wako, vitu unavyopenda kufanya na uwezo wako

Huduma katika kufanya mabadiliko kimasomo kwa wanafunzi

Teknolojia

Huduma za uhafifu wa kuona

Huduma za mafunzo ya awali na uwezo wa kujishughulisha  
Mafunzo ya kujirekebisha

## **Yote haya ni kuhusu kazi, kazi, kazi:**

DBVI inatoa ushauri wa kuweza kupata kazi katika fani mbali mbali, uratibu wa huduma, na msaada katika mipango mbali mbali inayoweza kukusaidia kupata kazi ya muda mrefu.

## **DBVI inatoa:**

Ushauri wa jinsi ya kujiendeleza kikazi  
Mafunzo ya fani mbali mbali  
Masomo ya juu  
Teknolojia ya kisasa  
Ujuzi wa kutafuta kazi  
Msaada unaotolewa na mwajiri  
Kuanzisha biashara ndogo ndogo  
Huduma ya utafutaji wa kazi

## **Kwa maelezo zaidi piga simu namba:**

**1-888-405-5005**

Email: [dbvi-info@state.vt.us](mailto:dbvi-info@state.vt.us)

Tovuti: [www.dbvi.vermont.gov](http://www.dbvi.vermont.gov)

## **Kushirikiana ili kutimiza malengo yako....**

DBVI – Idara ya vipofu na wasioona vizuri

Jimbo la Vermont